



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



JULAI 25, 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias Leo Julai 25, 2022 ameshiriki siku ya kumbukizi ya **MASHUJAA** iliyofanyika kiwilaya katika kata ya Luilo

Katika kumbukizi hiyo Askari wanafunzi wa Jeshi la akiba wakiongonzwa na Mkufunzi wa Jeshi hilo SSGT. Hussein Mchomvu na Msaidizi wake SGT Vuai Rajabu wanaoendelea na mafunzo katika kata ya Luilo wameshiriki shughuli mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na Kufanya usafi wa mazingira kwenye kituo cha Afya cha Luilo lakini kwenye mitaa yote ya kata hiyo.

Aidha vijana hao wakijumuika na wananchi kushiriki kumbukizi hiyo zaidi ya vijana 30 wamechangia damu salama kwa hiyari na zaidi ya watu 301 wamechanjwa chanjo ya UVIKO 19.

Wakati akiwapongeza vijana hayo kwa udhubutu na moyo wa uzalendo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa amesema kuwa *"binafsi niwapongeze vijana wote kwa moyo wa uzalendo kwenye Taifa letu, vijana wote ninyi zaidi 146 mpo hapa na mnatarajia kumaliza mafunzo yenu mwezi wa kumi na moja basi kama Mkurugenzi niwahakikishie kwamba miradi mikubwa inafunguka kwenye Halmashauri yetu kama vile ya makaa yamawe, huko wanahitaji walenzi hivyo nitaongea na makampuni ya ulinzi waanze kuwapa vipaumbele ninyi mlio malinza mafunzo.*

**Chrispin B. Kalinga**  
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini  
Halmashauri (W) Ludewa



**Jiandae Kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022**